TUSAHIHISHE MAKOSA: ANGAZIO LA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 TANZANIA

MUHTASARI

Waangalizi wa uchaguzi wa Oktoba 2020 nchini Tanzania walishuhudia idadi kubwa ambayo haijapata kutokea ya askari wa usalama kumwagwa mitaani, vikiwamo vikosi vya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi Tanzania (TPF), na vikosi vya wanamgambo vya chama na serikali, hususan katika visiwa vya Unguja na Pemba huko Zanzibar.

Magari ya kivita ya polisi yalifanya doria visiwani, ambako inasemekana vikosi vya usalama viliwaua raia kadhaa kwa kuwafyatulia risasi. Katika kipindi cha karibu na uchaguzi na siku kadhaa baadaye, kulikuwa na vikosi vingi vya usalama vilivyowatisha raia kote Zanzibar. Maafisa wa usalama waliwanyanyasa na kuwashambulia raia, ambao walihofia kuripoti matukio kama hayo kwa kuwa watu walioyatenda ni wale wale waliokuwa wamepewa jukumu la kulinda usalama na kupokea ripoti za vurugu.

Si tu kwamba idadi kubwa ya vikosi vya usalama ilisababisha kutanda kwa hali ya hofu lakini pia iliondoa haki ya kujumuika, na wakati mwingine ilisababisha mapambano makali na wananchi. Mara kwa mara vikosi vya usalama vilidhibiti maandamano ya wananchi kwa kutumia nguvu kupita kiasi kama vile mabomu ya machozi na risasi za moto.

Madai kamili ya ukiukaji wa haki za binadamu katika uchaguzi wa Oktoba 2020 yameelezwa kwa kirefu. Kulikuwa na ripoti kadhaa za watu kushambuliwa kimwili na kusababishiwa majeraha, kuteswa, kutekwa nyara, na kutiwa mbaroni na hata kuuawa. Vyama vya upinzani viliripoti wafuasi wao kushambuliwa, kutiwa mbaroni kiholela. Kufikia Novemba 2, 2020, wafuatiliaji wa haki za binadamu na wanasheria waliowakilisha vyama vya upinzani waliripoti kuwa zaidi ya watu 300 walikuwa wamekamatwa na vikosi vya usalama. Hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kuwawajibishwa waliojeruhi na kuua raia Tanzania Bara na Zanzibar.

Kutokana na taarifa hizi za awali, *SautiKubwa* na *Journalists For Justice* walipeleka waangalizi kote Tanzania kati ya Juni 2021 na Aprili 2022 kukusanya ushahidi na kuorodhesha matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu yanayohusiana na taarifa hizi za

kipindi cha uchaguzi. Kwanza waangalizi wa haki za binadamu walipewa mafunzo kuhusu ufuatiliaji wa haki za binadamu, kuorodhesha matukio na kutoa ripoti.

Walipelekwa katika mikoa 25 kati ya 31 ya Tanzania, ikiwamo Dar es Salaam, Ruvuma, Arusha, Shinyanga, Geita, Mbeya, Njombe, Iringa, Zanzibar, Kagera, Tabora, Mtwara, Simiyu, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Tanga, Kigoma, Songwe, Rukwa, Singida, Morogoro, Mwanza, Dodoma na Pemba. Ripoti hii inaangazia ukiukwaji wa haki za binadamu huko Zanzibar, Pemba, Songwe, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Kigoma, Songwe, Simiyu, Dar es Salaam, Rukwa, Ruvuma, Mara na Pwani. Waliwahoji watu 59 waliokuwa waathiriwa, manusura, mashuhuda, au wanafamilia na marafiki wa wahusika. Kwa kiasi kikubwa, walitafuta kuoanisha taarifa na nyaraka rasmi za taarifa kutoka vituo vya polisi, hospitali, na maafisa wa usimamizi na upigaji kura.

Pia, waangalizi walithibitisha taarifa walizokusanya kwa kulinganisha na picha za video, picha za watu binafsi, taarifa rasmi na ripoti za vyombo vya habari. Mkaguzi wa kujitegemea mwenye ujuzi wa sheria alichunguza picha zote. Matokeo yalioanishwa na kuwekwa katika mfumo wa simulizi.

Kwa kifupi, vifo mbalimbali vilitokana na majeraha ya risasi walizopigwa wakati polisi wakiyatawanya makundi ya watu na vifo vingine vilitokana na kuteswa. Vifo vingi vingeweza kuepukwa endapo majeruhi wangepatiwa matibabau mara moja, lakini hali ya usalama ilikuwa tete kiasi kwamba vituo vingi vya afya viliwakataa majeruhi wengi, na hata vile vituo vilivyowapokea havikuwapa msaada wowote. Katika baadhi ya matukio, vyombo vya usalama vilichochea vurugu kwa vyama vya upinzani ili kupata sababu ya kutumia nguvu kuvikabili kwa kisingizo cha kurejesha utulivu, na hatimaye kuishia tu kusababisha majeraha na vifo. Baadhi ya matukio yaliyosababisha vifo yalifanywa na raia, lakini pia hakuna yeyote aliyewajibishwa kwa hilo.

Wengi wa waliouawa ndiyo walikuwa tegemeo la familia kiuchumi, lakini sasa familia zao zimebaki yatima.

Waathitika wengine ambao walikuwa wakijulikana kwa baadhi ya maafisa wa usalama walitajwa kwa majina yao kabla ya kushambuliwa vikali na kujeruhiwa. Hivi sasa wanaishi wakiwa vilema bila ya msaada wowote rasmi wa kuwauguza.

Mara kwa mara wagombea na maafisa wa vyama vya upinzani walitiwa mbaroni, kuwekwa kizuizini, na hata kupelekwa mahakamani kwa mashitaka ya kubambikwa, yote hayo yakiwa ni sehemu ya njama za kuwazuia kushiriki katika uchaguzi. Wengine walishambuliwa kimwili, watoto wao walinyakuliwa na wao wenyewe walitekwa nyara na kuteswa bila serikali kuonesha nia yoyote ya kuwasaidia kupata fidia. Katika tukio moja, mgombea ubunge mwanamke aliyekwenda kutoa taarifa za kuwapo matukio yasiyoeleweka eneo la nyumbani kwake, yeye ndiye aliyetiwa mbaroni na kuzuiliwa usiku kucha bila kufunguliwa mashtaka.

Halikuwa jambo la ajabu kwa nyumba za wafuasi wa upinzani kupekuliwa kiholela na kuingiliwa faragha zao, ikiwamo kuingilia mawasiliano yao ya binafsi. Baada ya kushikilia vifaa vyao vya mawasiliano, hakuna mashtaka yoyote yaliyofunguliwa dhidi yao.

Huko Zanzibar, raia wengi walinyimwa haki yao ya kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi za uongozi kwa sababu hawakuwa na hati za kusajiliwa kama mkazi wa Zanzibar maarufu kama Kadi ya Mzazibari Mkaazi (ZAN ID). Sheria inamtaka mtu kuwa na hadhi ya kuwa mkazi ili kusajiliwa kama mpiga kura na kugombea katika uchaguzi Zanzibar. Uchaguzi wa Zanzibar umekuwa na mazoea ya vurugu, na waathirika wengi kwa vipindi kadhaa vya uchaguzi.

Ripoti hii inatoa wito kwa marais wa Tanzania na Zanzibar pamoja na vyombo vya serikali, akiwamo Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai na Jeshi la Polisi, kukubali ukiukaji uliobainishwa na kuchukua hatua za kusahihisha makosa. Pia, inatoa wito kwa mamlaka zinazosimamia uchaguzi nchini pamoja na Bunge kurekebisha sheria na taratibu zinazofanya ukiukaji kama huo kutokea. Ripoti hii pia inaitaka Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, na Shirika la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kupitisha maazimio yanayounga mkono matokeo ya ripoti hii na kulifikisha jambo hili kwa mamlaka za Tanzania.

- # Mapendekezo

- ## Mapendekezo kwa Rais Samia Suluhu Hassan
    - Hakikisha sheria na kanuni zote kandamizi zinafutwa na kufanyiwa mapitio ili kuzifanya ziendane na Katiba ya Tanzania na wajibu na ahadi za kimataifa za haki za binadamu.
    - Eleza ukweli na msingi wa kisheria kuhusu ukiukaji wa haki za binadamu uliobainishwa katika taarifa hii na ukubali mara moja kufanyika uchunguzi huru na usio na upendeleo kuhusu ukiukaji na matukio mengine yenye sababu za kuridhisha kwamba ukiukaji wa haki za binadamu ulifanyika.
    - Kubali kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kunakuwa na uchaguzi huru na wa haki, ikiwamo tume huru ya uchaguzi, kama ilivyopendekezwa katika ripoti mbalimbali ikiwamo ripoti ya Tume ya Uchaguzi (NEC) yenyewe pamoja na hukumu ya Julai 2020 ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu haki ya kupinga matokeo ya uchaguzi na kesi nyingine zinazoendelea mahakamani.
    - Karibisha na shirikiana na waangalizi na mifumo ya haki za binadamu, ikiwamo Tume ya Afrika na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu, ili kuchunguza kwa uhuru hali ya haki za binadamu nchini Tanzania ili kurekebisha hali iliyopo kuepuka vurugu zaidi katika siku za usoni.
    - Hakikisha ushiriki usio na upendeleo wa vikosi vya usalama katika uchaguzi wowote ujao kwa kuongozwa na kanuni thabiti ya mwenendo na maadili.

- ## Mapendekezo kwa Rais Hussein Ali Mwinyi
    - Hakikisha uchunguzi wa haraka wa matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu yaliyotokea Zanzibar, ambayo yameelezewa kwa kina na wahusika mbalimbali wa kimataifa na kitaifa yaliyosababisha kujeruhiwa vibaya na katika baadhi ya matukio vifo.
    - Hakikisha wote waliohusika na vurugu katika kipindi cha uchaguzi wa mwaka 2020 wanawajibika na kuwepo na fidia sahihi kwa waathirika wa vurugu hizo.

- Kubali kufanya mapitio ya haraka na kufuta vifungu visivyofaa vya Sheria ya Uchaguzi Na. 4 (2018), ambayo ilikuwa ndicho chanzo cha malalamiko mengi ya wadau mbalimbali katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa 2020.
- Karibisha na shirikiana na waangalizi huru wa haki za binadamu kutathmini hali ya haki za binadamu Zanzibar na pendekeza hatua stahiki za kusahihisha makosa na kufanya mabadiliko.

- **Mapendekezo kwa Wizara ya Sheria na Katiba**
  - Chunguza kikamilifu matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu yaliyobainishwa, ikiwamo watu kuuawa kinyume cha sheria, na kuweka wazi ushahidi wowote wa matukio yoyote ya aina hiyo ya ukiukaji wa haki za binadamu, hasa mauaji yaliyobainishwa kwenye ripoti hii, kwa umma.
  - Hakikisha mamlaka zinaheshimu kikamilifu na kwa dhati, zinalinda, zinaendeleza, na kutekeleza haki za binadamu za kila mtu, ikiwamo haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukutanika kwa amani.
  - Hakikisha kwamba waathirika na manusura wa ukiukaji wa haki za binadamu, wakiwamo wanafamilia wa waathirika wa mauaji, wanapata fursa ya kufidiwa kutokana na madhara waliyopata. Pale palipo na ushahidi wa kutosha, Serikali ya Tanzania inapaswa kuwafikisha mahakamani wahusika chini ya utaratibu wa mashtaka yanayozingatia haki.
  - Peleka Bungeni Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora kwa ajili ya kuidhinishwa.

- **Mapendekezo kwa mamlaka zinazosimamia uchaguzi Tanzania na Zanzibar**
  - Chukua hatua kuhakikisha kunakuwa na uchaguzi wa haki katika siku za usoni, ikiwamo kufanya uchunguzi huru, wa kina, wa wazi, na wenye ufanisi kuhusu tuhuma za uhalifu zilizosababisha ukiukwaji wa haki za binadamu wakati wa uchaguzi na kumwajibisha yeyote anayetuhumiwa kuhusika.
  - Peleka marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Na. 4 (2018) kwa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuhakikisha kunakuwa na uchaguzi ulio wazi zaidi na usimamizi wa kuwajibika wa uchaguzi.
  - Hakikisha kuwezesha uangalizi huru wa uchaguzi kwa waangalizi wa kitaifa na kimataifa kupitia mchakato wa wazi na uwajibikaji wa uhakiki wa kura.
  - Wawajibishe wafanyakazi wa mamlaka zinazosimamia uchaguzi waliotuhumiwa katika vitendo mbalimbali vya ukiukaji uliochangia kuleta kasoro za uchaguzi wa mwaka 2020.
  - Ahidi kutekeleza uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ya kuhakikisha uchaguzi huru, wa haki na jumuishi kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu pamoja na Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora.

- **Mapendekezo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
  - Futa marekebisho yenye utata kwenye sheria za uchaguzi yanayozuia wananchi kupata kikamilifu haki zao za msingi wakati wa uchaguzi. Hii ni pamoja na haki ya

uhuru wa kujieleza unaofinywa na Sheria ya Makosa ya Mtandao (2015), Sheria ya Uchaguzi Tanzania (Cap 343), Sheria ya Serikali za Mitaa (Uchaguzi) (Cap 242), na Sheria ya Vyama vya Siasa (Marekebisho) (2019).
- Futa sheria zote zinazoruhusu kunyimwa dhamana kabla ya kesi kusikilizwa kwa watu wote wanaoshitakiwa, dhamana kabla ya kesi kusikilizwa, na dhamana kabla ya rufani kusikilizwa.
- Unda kamati ya uchunguzi ya bunge kuhusu mwenendo wa uchaguzi wa mwaka 2020 na toa mapendekezo stahiki ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Serikali kuhakikisha kunakuwa na uchaguzi huru na wa haki katika siku za usoni. Idhinisha Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora.

- **Mapendekezo kwa Jumuiya ya Kimataifa, na wabia wa maendeleo**
  - Dai kwa bidii kufanyika kwa uchunguzi na uwajibikaji kwa ukiukwaji wa haki za binadamu uliobainishwa kuhusu uchaguzi wa Oktoba 2020 nchini Tanzania.
  - Ahidi kufanyika mazungumzo ya watu wote na ya wazi na Serikali ya Tanzania kuhusu hali ya haki za binadamu na demokrasia, ikiwamo ukiukwaji uliobainishwa katika uchaguzi wa mwaka 2020.
  - Hamasisha na endeleza mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania na asasi huru za kiraia, pamoja na waangalizi wa haki za biandamu wa kitaifa na kimataifa.
  - Tumia nguvu ya ushawishi wa kusaidia maendeleo nchini Tanzania ili kubaini na kuweka vigezo vinavyoeleweka vya kuzingatia haki za binadamu.
  - Pigia chapuo Mfumo wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa kuhusisha kwa bidii uzingatiaji wa haki za binadamu katika mipango ya maendeleo ya Tanzania.
  - Unga mkono juhudi za asasi huru za kiraia, yakiwamo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) ya kitaifa na kimataifa, kuchunguza na kufuatilia hali ya haki za binadamu nchini na kutaka kuwe na uwajibikaji.

- **Mapendekezo kwa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu**
  - Fanya mapitio ya hali ya haki za binadamu nchini Tanzania kabla, wakati, na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020, na pitisha azimio la kulaani ukiukwaji wa haki za binadamu na ukatili uliofanyika kabla, wakati, na baada ya uchaguzi kwa lengo la kuhakikisha haki inatendeka kwa waathirika.
  - Eleza wasiwasi na mapendekezo yaliyoelezewa hapo juu katika mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na himiza utekelezaji wake mara moja.
  - Fanya ziara maalumu nchini Tanzania ili kufanya tathmini binafsi ya hali ya haki za binadamu na pendekeza hatua stahiki za marekebisho kabla ya uchaguzi ujao.
  - Andaa kikao maalumu kuhusu Tanzania ili kufanya mapitio ya hali ya haki za binadamu kufuatia matamko ya hivi karibuni ya Tume na Wajumbe Maalumu wa Umoja wa Mataifa (UN Special Rapporteurs) ili kutathmini hatua zinazochukuliwa kurekebisha udororaji wa hivi karibuni wa hali ya haki za binadamu.

- **Mapendekezo kwa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu**

- Fanya mapitio ya hali ya haki za binadamu kabla, wakati, na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020 na pitisha azimio kulaani ukiukwaji wa haki za binadamu na ukatili uliofanyika kabla, wakati, na baada ya uchaguzi kwa lengo la kuhakikisha haki inatendeka kwa wahanga.
- Eleza wasiwasi na mapendekezo yaliyoelezewa hapo juu katika mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na himiza utekelezaji wake mara moja.
- Omba na fanya ziara maalumu nchini Tanzania kutathmini hali ya haki za binadamu kufuatia matamko kadhaa ya Wajumbe Maalumu wa Umoja wa Mataifa (UN Special Rapporteurs) na mifumo mingine na pendekeza hatua za marekebisho kabla ya uchaguzi ujao.
- Pendekeza kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kufanyika kikao maalum kuhusu Tanzania ili kujadili hali ya haki za binadamu nchini na hatua zinazochukuliwa kuondokana na udororaji wa hivi karibuni.